Australian Government
Australian Digital Health Agency

My Health Record

Udhibiti wa anayeweza kuangalia habari zako za Rekodi ya Afya Yangu (My Health Record)

Rekodi ya Afya Yangu ni muhtasari salama ulioko katika mtandaoni wa habari yako ya afya.

Unaweza kudhibiti kile kilicho kwenye Rekodi ya Afya Yangu na nani anayeweza kuona maelezo yako.

Habari ya Rekodi ya Afya Yangu haipatikani kwenye mtandao wa wazi. Wahudumu wa afya wanapaswa kusajiliwa ili kutumia Rekodi ya Afya Yangu kwa kutumia mfumo wa kompyuta salama.

Ni kinyume na sheria kwa mtu kutazama kwa makusudi rekodi yako isipokuwa ni kwa ajili ya kukupa huduma za afya. Kuna adhabu kubwa kwa kuangalia habari hizi kwa haramu.

Unaweza kuweka nambari za siri ili kulinda habari yako ya afya

Mfumo wa Rekodi ya Afya Yangu Umejengwa ili kufanya habari yako ya afya ipatikane kwa ulinzi na salama. Wahudumu wa afya wanaokupa huduma za matibabu ndio wanaweza kuangalia Rekodi yako ya Afya. Ikiwa unataka usiri wa ziada, unaweza kuweka nambari za siri au kufuta nyaraka na maelezo ya Medicare kutoka kwa rekodi yako wakati wowote.

Kuweka Rekodi Nambari ya kuingia au nambari ya siri (Record Access Code) (RAC) huzuia wahudumu wa afya kuwa na uwezo wa kuangalia Rekodi yako ya Afya. Unapoweka (RAC), unaweza kuwatolea nambari ya siri kwa watoa huduma wako wa afya ikiwa unataka waweze kuangalia habari yako ya Rekodi ya Afya.

Unaweza kubadilisha nambari ya siri wakati wowote kwa kuingia kwenye rekodi yako ya Afya kupitia mtandaoni.

Muhimu: Baada ya mhudumu wa afya kuangalia rekodi yako ya afya, mhudumu huyo anaongezwa kwenye Orodha ya Watoa Huduma za Afya (Healthcare Provider Access List) katika Rekodi ya Afya Yangu. Hii inamaanisha kwamba hata kama utaweka (RAC) kwenye rekodi yako, wahudumu wa afya ambao wameangalia rekodi yako bado wataweza kuiangalia bila kutumia nambari ya siri.

Ikiwa unataka wahuduma hao kuzuiwa kuona rekodi yako, unahitaji kuwaondoa kwenye Orodha ya Watoa Huduma za Afya.

Kuweka Nambari ya Kuingia/siri kwa Nyaraka ya kizuizi (Limited Document Access Code) (LDAC) huzuia watoa huduma za afya kuwa na uwezo wa kuangalia hati flani ndani ya rekodi yako.

Unapoweka (LDAC), unaweza kuwatolea nambari ya siri kwa watoa huduma wako wa afya ikiwa unataka waweze kutazama nyaraka hizo.

Katika wakati wa dharura, udhibitishi wako wa Rekodi yako ya Afya Yangu unaweza kuzimwa kwa muda. Hii ina maana kuwa watoa huduma za afya wanaokuangalia wanaweza kuona haraka mawasiliano yako ya dharura, madawa na chanjo. Hii huwasaidia kukupa matibabu kwa ustawi salama, bila ya kungojea Udhibitishi wako au nambari yako ya siri.

Ni kinyume na sheria kwa mtu kutazama kwa makusudi rekodi yako isipokuwa ni kwa kukupa huduma za afya. Kuna adhabu kubwa kwenye sharia ikiwa faini nzito na kupelekwa jela.

MyHealthRecord.gov.au
Piga 1800 723 471

Jinsi ya kudhibiti hatua kwa hatua

Jinsi ya kupata udhibiti

Tumia MyGov kuangalia Rekodi Yako ya Afya. Ikiwa huna akaunti ya MyGov, nenda kwenye mtandao wa https://my.gov.au ili kufungua akaunti. Baada ya kuingia kwenye MyGov, chagua 'Services' (Huduma), baadaye chagua kitufe cha 'Link' ili kufungua Rekodi ya Afya Yangu. Utahitaji kujitambulisha mwenyewe kwa kujibu mfululizo wa maswali kuhusu ziara yako ya mwisho kwa mhudumu wa afya.

Jinsi ya kufunga na Nambari ya Siri (RAC)

Ingia kwenye rekodi Yako ya Afya kupitia myGov

1. Chagua 'Privacy & Access "Usiri na kuingia'



2. Kwenye 'Document Access Setting "Mpangilio wa Nyaraka ya Kuingia' chagua kitengo cha 'Manage Access "Dhibiti Kuingia'



3. Listi ya kwenda chini itatokea. Chagua 'Manage Access "Dhibiti Kuingia' kutoka kwenye listi



4. Weka nambari za siri (urefu wa nambari 4 hadi 8), baadaye chagua 'Continue "Endelea' na 'Confirm "hakikisha'.

   Nambari hii ya siri haiwezi kuwa sawa na ile Nambari ya Siri ya Nyaraka ya Kizuizi (LDAC), kama unayo Rekodi ya Kizuizi.





Kama unahitaji msaada wa zaidi kuweza kufungua rekodi ya Afya Yangu, unaweza wasiliana na sisi kupitia nambari hii 1800 723 471

Jinsi ya kuondoa daktari kutoka kwa Orodha ya Watoa Huduma za Afya katika Rekodi Yako ya Afya kupitia MyGov

Ingia kwenye rekodi Yako ya Afya kupitia myGov

1. Chagua ‘Privacy & Access “Usiri na Kuingia’



2. Katika ‘Document Access Setting “Mpangilio wa Nyaraka ya Kuingia’ chagua kitengo cha ‘Manage Access “Dhibiti Kuingia’



3. Listi ya kwenda chini itatokea. Chagua ‘Manage Access “Dhibiti Kuingia’ kutoka kwenye listi



4. Chagua ‘Remove “Ondoa’, baada ya kuondoa mhudumu chagua ‘Continue “Endelea’ na ‘Confirm “hakikisha’.





Jinsi ya kuweka Nambari ya Siri Kwenye Nyaraka ya Kizuizi (LDAC)

Ingia kwenye rekodi Yako ya Afya kupitia myGov

1. Chagua 'Privacy & Access "Usiri na Kuingia'



2. Katika kitengo 'Access by Healthcare Providers "Kuingia kwa Watoa Huduma' chagua 'Manage Access "Dhibiti Kuingia'



3. Chagua 'Set limited document access code "Weka Nyaraka ya Kizuizi Nambari ya Siri ya Kuingilia'



4. Weka nambari za siri (urefu wa nambari 4 hadi 8), baadaye chagua 'Continue "Endelea' na 'Confirm "hakikisha'.

   Nambari hii ya siri haiwezi kuwa sawa na ile Nambari ya Siri ya rekodi ya Afya Yangu.





5. Tafuta nyaraka unayotaka kuzuia uingiaji, changua 'Manage Access "Dhibiti Kuingia'